

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA
Simu Na: +255 26 2321607
Nukushi: +255 26 2322116
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Mji wa Serikali – Mtumbwa,
Mitaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI NA
SEKONDARI**

A: UTANGULIZI

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inapenda kuutangazia Umma kuwa Serikali imetoa nafasi za ajira ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Kwa sababu hiyo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inawatangazia walimu wenyewe sifa kutuma maombi yao kwa njia ya mtandao kuitia kiunganishi cha ajira.tamisemi.go.tz (*Online Teacher Employment Application System - OTEAS*).

Walimu wanaotakiwa kutuma maombi ni wenyewe sifa za kitaaluma kama ifuatavyo:

B. WALIMU WA SHULE ZA MSINGI

- i. Mwalimu Daraja la IIIA – mwenye Astashahada (Cheti) ya Ualimu;
- ii. Mwalimu Daraja la IIIB - mwenye Stashahada (Diploma) ya Ualimu katika somo la *English* na waliosomea *Elimu ya Awali*;
- iii. Mwalimu Daraja la IIIC - mwenye Shahada ya Ualimu wa masomo ya *English, Civics, General Studies, History, Geography na Kiswahili*;
- iv. Mwalimu Daraja la IIIB na IIIC – mhitimu wa Stashahada (Diploma) ya Ualimu (Elimu Maalum) wa masomo ya Lughu, Sanaa, Sayansi na Hisabati.

C. WALIMU WA SHULE ZA SEKONDARI

- i. Mwalimu Daraja la IIIB – mwenye Stashahada (Diploma) ya Ualimu waliosomea Elimu Maalum kwa masomo ya *English Language, Geography, Physics na Mathematics*;

- ii. Mwalimu Daraja la IIIB – mwenye Stashahada (Diploma) ya Ualimu wa masomo ya *Physics, Mathematics, Biology, Chemistry, Home Economics* na *Agricultural Science*;
- iii. Mwalimu Daraja la IIIC – mwenye Shahada ya Ualimu waliosomea Elimu Maalum kwa masomo ya *English Language, Geography, Physics* na *Mathematics*;
- iv. Mwalimu Daraja la IIIC - mwenye Shahada ya Ualimu wa masomo ya *Physics, Mathematics, Chemistry* na *Biology*.
- v. Mwalimu Daraja la IIIC - mwenye Shahada ya Ualimu wa masomo ya *Agricultural Science, English Language, English Literature, Chinese, French, Book Keeping, Commerce, Accounts, Economics* na *Home Economics/Food and Human Nutrition*;
- vi. Wahitimu wa Stashahada (Diploma) ya Ufundi na Shahada ya Uhandisi Ujenzi (*Civil Engineering*), Uhandisi Mitambo (*Mechanical Engineering*), Uhandisi Umeme (*Electrical Engineering*) na *Electronic Engineering* ambao wataajiriwa kama Walimu Daraja la IIIB na Daraja la IIIC; na
- vii. Fundi Sanifu Maabara - wahitimu wa Stashahada (Diploma) ya Ufundi Sanifu Maabara na Stashahada ya Sayansi na Teknolojia ya Maabara.

D. SIFA ZA JUMLA ZA MWOMBAJI

Mwombaji wa nafasi zilizoainishwa hapo juu awe na sifa za jumla zifuatazo:-

- i) Awe ni Mtanzania;
- ii) Awe amehitimu kati ya **mwaka 2014 hadi 2019**.
- iii) Asiwe na umri wa zaidi ya miaka arobaini na tano (45);
- iv) Walimu waliowahi kutuma maombi na hawakupata nafasi za ajira wanaweza kutuma maombi upya;
- v) Walimu waliowahi kuajiriwa **Serikalini** hawatakiwi kutuma maombi; na
- vi) Kila mwombaji wa ajira ya Ualimu ahakikishe ana Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya NIDA.

E. MWISHO

Maombi yote ya ajira yatumwe kupitia kwenye mfumo wa maombi ya ajira wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ulivyooneshwaa kwenye tangazo hili. Hakuna maombi yatakayopokelewa kwa njia tofauti na iliyoelekezwa. Waombaji wanatakiwa kutuma maombi yao kuanzia tarehe **07/09/2020** hadi **21/09/2020**.

Imetolewa na:

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais – TAMISEMI.
DODOMA.

7 Septemba, 2020